

MLUTHERI NI NANI?

Kiasili, Mlutheri ni mfuasi wa Martin Luther. Si kweli! Sisi ni wafuasi wa Yesu Kristo. Martin Luther ni kama vile wewe na mimi ni vyombo vya kidunia kubeba hazina ya injili kwa ulimwengu. Kwa pamoja, udongo wa dhambi unaopita hazina ya utukufu umekuwa umekombolewa katika Yesu. Tunaamini kama Martin Luther kwamba tunaokolewa:

Kwa neema tuu, Kwa imani tuu, Kwa Kristo tuu, Kwa neno tuu.

Tunatumia jina la Martin Luther kutofautisha na makanisa mengine ya ukristo. Na kwa zaidi kutofautisha na wengine ambao wanavaa jina la “Kilutheri” Tunajiita kanisa la ukiri wa Kilutheri.

Tunaokolewa kwa neema tuu.

Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu. (Efeso 2:8-9)

Neema ni upendeleo usiostahili au upendo ambao haukustahili. Iitolewa kwetu katika Kristo Yesu na kwa wokovu amefanya kwa ajili yetu. Hatuwezi kufanya kitu chochote kuipata mbingu. Ni zawadi ya bure katika Kristo. Kwa hiari alikuja ulimwenguni na kuishi maisha makamilifu ambayo hatungezeza. Wakati alipofanya hili alitimiliza sheria kamilifu ya Mungu. Mungu husema, “Mtakuwa wakamilifu kwa kuwa mimi Bwana Mungu wako ni Mkamilifu” Hakika sisi siyo wakamilifu. Hivyo Yesu wetu alikuja na kuishi maisha makamilifu badala yetu. Hivyo Mungu alistahili adhabu ya dhambi. Kama ukivunja mojawapo ya sheria wewe ni mwenye hatia. Roho itendayo dhambi ndiyo itakayokufa. Siyo tuu Yesu aliishi maisha matakatifu katika sehemu yetu, lakini alikufa akachukua adhabu yetu juu yake. “Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, akachubuliwa kwa maovu yetu; adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, na kwa kupigwa kwake sisi tumepona” (Isaya 53:5), Alifanya hili kwa wale ambao hawakustahili. Ni upendo wa jinsi gani alionao juu yetu sisi wenye dhambi!

Wakati alipokufa juu ya msalaba alsema, “Imekwisha,” kazi ya kuokoa ulimwengu huu uliopotea imekamilika. Mungu alihitaji ukamilifu na Yesu alikuwa Mwanakondoo mkamilifu wa Mungu. Mungu alihitaji kuiadhibu dhambi na alimtuma mwanawe pekee kubeba dhambi ile.

Sasa kama Paulo alivyoandika, “Ni kipawa cha Mungu,” wokovu huu ulitolewa na Yesu. Vipi kama mtu Fulani akija katika mlango wako na dola milioni moja? Hukujua kama angekuja. Ulikuwa mvivu na ulikuwa hufanyi kazi wakati ule fedha zikaja moja kwa moja kwako. Hukuzifanyia kazi. Hakika hukuzistahili. Hivyo ni kama wokovu ndani ya Yesu. Ni zawadi safi na rahisi kutoka katika mkono wa fadhili wa Mungu wako mwenye upendo. Kama ungepaswa kufanya kazi maisha yako yote usingeweza kustahili.

Kwa huzuni leo kuna watu wanofundisha kwamba tulistahili kuifanyia kazi na kuwa nayo, ingawa

ni kwa sehemu. Sababu ya matengenezo ya Lutherani ilikuwa kanisa limetekwa na Upapa ambao uliofundisha kuwa tunaokolewa kwa neema na matendo. Biblia hufundisha kuwa tunaokolewa kwa neema, na kama ni kwa neema ya Mungu hivyo siyo kwa matendo. Hivyo Mungu alitumia matengenezo (Reformation) kuwarudishia watu wake fundisho la kweli na wokovu kwa neema tuu. “Wanahesabiwa haki bure kwa neema yake, kwa njia ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu” (Warumi 3:24).

Kanisa la Kikatoliki hufundisha hivyo na wanafundisha kwamba Mariamu na waumini wengine waliojikusanyia vya kutosha katika maisha yao wenyewe kufuta dhambi zilizotendwa katika maisha. Kama maana ni kweli, husema, hawa walijikusanyia zaidi vya kutosha kustahili wao wenyewe. Unaweza kuomba kuwa na baadhi ya kustahili kwao ni upuuzi wa namna gani! andiko huweka wanadamu wote pamoja kama watenda dhambi katika kuhitaji wokovu, siyo kuhitaji sehemu ya wokovu kutoka kwa Mungu na sehemu nyingine iondolewe na mwanadamu kwa kuwa hakuna utofauti. Ni haki ya Mungu iliyo kwa njia ya imani katika Yesu Kristo kwa wote waaminio. Maana hakuna tofauti; kwa sababu wote wamefanya dhambi, nakupungukiwa na utukufu wa Mungu (Warumi 3:22-23).

Kwa sababu ya Kanisa Katoliki kuandika katika fundisho la wokovu kwa neema tu tunabakia tumejitenga na kanisa hilo, tunajiita wenyewe ni “Lutherani” kwa sababu tunaamini kama Luther alivyofanya, Neno.

Tunaokolewa kwa imani tuu.

Basi twaona ya kuwa Mwanadamu huhesabiwa haki kwa imani pasipo matendo ya sheria. (Warumi 3:28). Ilikuwa ni kupitia kujifunza kwake kwa sehemu kitabu cha Warumi na Wagalatia kwamba Martin Luther aliposhikwa na nguvu ya Roho kwamba tunaokolewa kwa imani tuu. Tuna haki na wema katika macho ya Baba kupitia sifa njema na ridhaa ya Mwana. Haki ya Mwana hutufunika na kufanya juu yake dhambi zetu na kuwa na haki. Wakati Baba atuona kupitia Kristo, Mwokozi wetu, anawaona watoto wake mwenyewe. Tuna haki ya Kristo kwa imani, “hali ya Mungu kupitia imani iliyo katika Yesu Kristo kwa wote ambao huamini.” (Warumi 3:22). “Huhesabiwa haki kwa neema yake kama zawadi, kupitia ukombozi ulio katika Kristo, ambaye Mungu aliweka mbele kama kufidia kosa kwa damu yake, kupokelewa kwa imani. (Warumi 3:24-25). Tunapokea kipawa cha wokovu kwa imani. Hatuitendei kazi wala kuistahili. Tungeweza kusema kwamba imani ni mkono wa kupokea kipawa cha wokovu. Ndivyo ilivyo na siyo zaidi kama dunia kupokea Mwana.

Fundisho la uongo limeingia katika Kanisa kwamba imani siyo kitendo cha Mungu juu ya Mwanadamu, lakini angalau kwa sehemu mtu alivuviwa tunaamini inavyokiriwa katika Katekismo ndogo ya Martin Luther; “Naamini kwamba siwezi kwa sababu yangu au kwa nguvu kuamini katika Kristo Yesu, Bwana wangu, wala kuja kwake, “Lakini Roho Mtakatifu aliniita kwa injili, alinielimisha kwa karama zake, kunitakasa na kuniweka katika imani ya kweli; Kama namna aitavyo, hukusanya, kuelimisha na kutakasa kanisa lote la Kikiristo duniani; na kuliweka pamoja na Yesu Kristo katika imani moja ya kweli....” Kama ni kwa sababu yeyote au nguvu kati yangu

mwenyewe kwamba naamini ,hivyo siyo tena kwa neema tuu.Imani kiurahisi ni mkono wa kupokea unaoweza kwa Roho.

Kama Walutheri hujitenga wenyewe kutoka makanisa mbalimbali ya Kikristo ambayo yanatoa maana ya Mwanadamu kuamini.Baadhi wanazungumzia uamuzi wao kwa Kristo kanakwamba ilikuwa kazi yao.Kweli ni kwamba kama Yesu alivyowaambia wanafunzi wake “Hamkunichagua bali niliwachagua.”Wengine wanasema kwamba sababu yawengine kuamini ni kwamba walikuwa wakielekeza kuamini, Kwamba walimkana Roho Mtakatifu kidogo kuliko wengine.Hii ni sababu ya kutoa sehemu ya sifa kwa kubadilishwa kuwa mtu mwenye dhambi.Mtume Paulo alielekeza kuamini? au je alimkataa Roho Mtakatifu kidogo kuliko wengine? Jibu ni hapana! Yeyote hawezi kumtafuta mtu ambaye kwa uchungu alipigwa njiani.Alisukumizia nje matishio na mauaji. “Sauli akaliharibu Kanisa, akiingia kila nyumba, nakuwaburuta wanaume na wanawake na kuwatupa gereza.Matendo 8:3”Ilikuwa ni nguvu za Mungu kwamba Sauli, mwenye kuudhi, kufanyika Paulo, Mtume na Mmisionari.

Baadhi yawengine wanasema kwamba mwanadamu “hushirikiana” na Mungu katika kubadilishwa kwake.Mtu asiye wa kiroho atakuwa mjinga hasa kwa mambo ya kiroho.Kutobadilika ni kifo katika dhambi.(Waefeso 2:1).Mtu asiye wa kiroho hapokei vipawa vya Roho Mtakatifu wa Mungu,Kwa sababu ni upuuzi kwake na hawezi kuwaelewa kwa sababu yanatambulika kiroho.(1 Wakorintho 2:14).Kama vile,katika siku ya mwisho itakuwa haswa nguvu ya Mungu kwamba wafu watakuwa wamefufuliwa,hivyo kubadilishwa ni kwa nguvu ya Mungu kwamba mfu wa kiroho anafanywa hai katika Kristo.

Hakuna mtu anayeweza kusema kwamba Yesu ni Bwana,lakini kwa Roho Mtakatifu.Chombo chake ni neno,upanga wa Roho.Ni Roho huita,hukusanya,huelimisha na kutakasa .Kama Walutheri,tunaamini kutoka katika andiko kwamba imani ni Roho iliyofuliwa .Na imani hii ni kipawa cha Mungu,kama ilivyo hakika ya wokovu wenyewe ulivyo.Kupitia imani,imani hii iliyofuliwa,na siyo matendo,kwamba tuliokolewa.

Tunaokolewa kwa Kristo tu.

“Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, Kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo. Matendo 4:12”Maandiko yote yanathibitisha kuwa Yesu ni Mwokozi wa ulimwengu.Alitimiliza unabii wa Agano la Kale kutoka Mwanzo 3:15 hadi Malaki 4:12.Ni mwanzo na mwisho .Ni yeye ambaye ni Emanueli wetu, Mungu pamoja na sisi.

Hata hivyo maandiko ni wazi sana ingawa wakristo wengi wa dhehebu,Romani Catholiki,,wana mpatanishi,Mariamam,kuomba na mwana wake.Mwokozi ni mwokozi.(1 Timotheo 2:5).Yesu alitoa wokovu kwa ajili yetu,hatia zetu ziliwekwa juu ya Bwana.Mariamam hakuwa na tofauti na mwenye dhambi yeyote,isipokuwa ni kwamba kwa neema safi ya Bwana alimchagua kumzaa mwana wa Mungu.hana msaada mbele ya kiti cha Mungu isipokuwa kupitia damu na usitahili wa mwana wake,Mwokozi wetu.Huyu ni sawa na sisi.Mwanakondoo wa Mungu ni pekee mwenye kustahili

kuchukua dhambi za ulimwengu. Kanisa la kweli la Kilutheri hufundisha katika siku za Luther na sasa kwamba Kristo ni wokovu tu. Kupitia yeye pekee tunamkaribia Baba wa mbinguni.

Katika siku hizi za mwisho kuna madhehebu mengi ambayo yana udhanio wao (Kristo) Yesu katika mlima wa mizeituni aliwaelekeza akiwaonya jinsi atakavyorudi “Nakama siku hizo zisingalifupishwa, asingeokoka mtu yeyote, lakini kwa ajili ya wateule zitafupishwa siku hizo. Wakati huo mtu akiwaambia, tazama, Kristo yupo hapa au yupo kule msisadiki. Kwa maana watatokea makristo wa uongo na Manabii wa uongo nao watatoa ishara kubwa na maajabu, wapate kuwapoteza kama yamkini, hata waliowateule. tazama, nimekwisha kuwaonya mbele. Mathayo 24:22-25” Yohana anawaita hawa kuwa “wapinga Kristo” kwa sababu wanajaribu kusimama sehemu ya Kristo. (1 Yohana 2:18-25; 4:1-6) Sisi Walutheri tunaamini, kufundisha na kukiri kwamba hakuna jina jingine walilopewa wanadamu litupasalo kuokolewa kwalo isipokuwa Yesu Kristo. Yeye pekee aliyefanya amani yetu kwa Mungu kupitia damu ya msalaba wake (Wakolosai 1:20; 2 Wakorintho 5:18-21) Soma wakolosai moja, Waebrania moja na Yohana moja utaona kuwa hakuna kushirikiana na yeyote Uungu wake.

Ilikuwa kazi ya Mungu kumwokoza mwanadamu, Yesu ni Mungu kweli na alifanya wokovu mkamilifu kwa mwanadamu. Tunawafundisha watoto wetu kutoka katika Katekismo ndogo, “Ninaamini kwamba Yesu Kristo, Mungu kweli, Mwana pekee wa Baba kutoka umilele, na pia mwanadamu kweli, aliyezaliwa na bikira Mariamu, Ni Bwana wangu; ambaye amenikomboa niliyepotea na kiumbe aliyelaumiwa, Alininunua na kuniokoa kutoka katika dhambi zote, kutoka katika kifo, na kutika katika nguvu za shetani, siyo kwa dhahabu au fedha, lakini kwa damu yake safi takatifu na kwa mateso na kifo cha asiye na hatia; kwamba niweze kuwa mali yake”

Tunaokolewa kwa neno tu.

“Kwa maana neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo. Waebrania 4:12

Hatuokolewi kwa kufuata au kuamini “mapokeo” kama yalivyoshikwa na wanadamu. Hatuendi mbinguni kwa sababu kile Mapapa na baraza la kanisa lilisema. Hatuna msamaha wa bure wa dhambi kwa sababu kikundi cha wanadamu katika kusanyiko walivyopiga kura. Tunaokolewa kwa kuliadini neno ambalo hutufanya wenye hekima katika wokovu. Wimbo wa zamani mmoja, ulisema mkono wa mwanadamu utakuangusha haupaswi kujiamini wewe mwenyewe. Kujifunza juu ya mwanadamu ni kama kujifunza hatua ya silaha. Kama wanadamu watasema neno la Mungu, Hivyo ni neno la Mungu kwamba huokoa na siyo la wanadamu.

Biblia ni neno la Mungu. Korani siyo neno la Mungu wala chochote kiitwacho ambacho kinaaitwa maandiko matakatifu ya namna yeyote ya Dini. “Kila andiko lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kuwaongoza, na kwa kuadibisha katika haki; Ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema. 2 Timotheo 3:16-17” Kwa kifungu hiki na vingine tunaona kwa maana Biblia ya Kikristo ni neno la kweli la Mungu na

kutofunga ukweli wa wokovu.Kama ulikuwa unasoma kitabu chochote kinachoitwa cha dini yeyote,vyote vina njia sawa ya wokovu,vimetajwa kupitia matendo.Ni katika neno la Mungu tu kwamba ni kwa njia ya neema,kwa imani,kwa Kristo. “Nasi tuna lile neno la unabii lililo imara zaidi,ambalo,nikiliangalia,kama taa ing’ aayo mahali penye giza mwafanya vyema,mpaka kutakapopambazuka,na nyota ya asubuhi kuzuka mioyoni mwenu.(2 Petro 1:19).

Biblia ni neno la Mungu kwa sababu ndani yake tumefunuliwa mwokozi, Yesu.Biblia kwa kweli ni habari zake.Kutoka katika injili ya kwanza ya ahadi katika mwanzo 3:15 tuna Yesu aliyefunuliwa.Ni uzao wa Mwanamke ambaye atamponda shetani kichwa.Shetani angeweza kumponda Yesu katika kisigino wakati ule Yesu aliposulibiwa katika mikono ya watu wenye dhambi.Lakini baada ya kufa alifufuka kutoka kwa wafu.

Yesu pia aliitwa neno la Mungu sawasawa na Biblia katika habari yake. “Hapo mwanzo kulikuwako neno,naye neno alikuwako kwa Mungu,naye neno alikuwa Mungu;Naye neno alifanyika Mungu akakaa kwetu;Nasi tukauona utukufu wake utukufu kama wa mwana pekee atokaye kwa Baba;amejaa neema na kweli”(Yohana 1:1;14).Wakati tunapolisoma neno tunalishikilia utukufu wa neno aliyefanyika Mungu.Bwana wetu anapotutia moyo kusoma neno kwa sababu “yanamshuhudia(Maandiko)”Yohana 5:39.

Tunaishi katika ulimwengu wa giza la namna hiyo.Ni kwa kupitia kulisoma na kujifunza neno kwamba tuweze kuwa na mwanga wa kweli duniani.Biblia ni taa ya miguu yetu na mwanga wa njia zetu,kwa sababu njia ya wokovu imefunuliwa kwetu kupitia neno ili tweeze kuamini.Na neno ni dhahiri katika umakini huu.

Mlutheri ni nani? Mlutheri ni mkristo ambaye anaamini kuwa tumeokolewa:

KWA NEEMA TU.

KWA IMANI TU

KWA KRISTO TU

KWA NENO TU

Kwa Mungu tu anapaswa sifa zote.